**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA**

# TAARIFA KWA UMMA

## TAARIFA YA UGONJWA WENYE DALILI ZA HOMA INAYOAMBATANA NA KUVUJA DAMU KATIKA HALMASHAURI YA RUANGWA MKOA WA LINDI

**18 JULAI 2022, RUANGWA – LINDI**

**Ndugu wananchi**

Itakumbukwa kuwa tarehe 07 Julai 2022, Wizara ya Afya ilipokea taarifa kutoka kwa Mganga Mkuu wa Mkoa wa Lindi ya uwepo wa wagonjwa wenye dalili za homa inayoambatana na kutoka damu katika Wilaya ya Ruangwa Mkoani Lindi. Kufuatia taarifa hizo, Wizara ilituma timu ya wataalam kutoka ngazi ya Wizara na wengine kutoka Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi (MUHAS), Chuo kikuu cha Mzumbe, Wataalam kutoka Timu za Usimamizi wa Huduma za Afya Mkoa wa Lindi na Halmashauri za Kilwa na Ruangwa pamoja na wataalam wa Mifugo wa Halmashauri za Ruangwa na Kilwa ili kufanya uchunguzi wa ugonjwa huu. Aidha tulipata ushiriki wa wataalam kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO) pamoja na kituo cha kudhibiti na kuzuia magonjwa cha Marekani (US CDC).

**Ndugu wananchi,**

Hadi kufikia siku ya tarehe 17 Julai 2022, jumla ya wagonjwa 20 na vifo vya watu watatu (3) vimetolewa taarifa. Aidha, kwa sasa, wagonjwa wawili pekee wenye dalili ndiyo bado wamelazwa katika eneo lililotengwa kwa ajili ya matibabu. Vile vile, timu zimeendelea na ufuatiliaji wa watu waliotangamana na wagonjwa (contacts) ambapo mpaka sasa, hakuna aliyeonesha dalili za ugonjwa huu.

**Ndugu wananchi**

Itakumbukwa kuwa, taarifa ya awali ya sampuli zilizopimwa katika Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii (National Public Health Laboratory) zilionesha majibu **hasi (negative)** kwa ugonjwa wa **Ebola, Marburg na UVIKO-19**. Vile vile, uchunguzi zaidi ulioendelea kwenye Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii na Wakala wa Maabara ya Mifugo umeonesha majibu **hasi (*negative*)** kwa ugonjwa wa ***Influenza, Kimeta (Anthrax), Crimean Congo Hemorrhagic Fever (CCHF), Yellow Fever, Chikungunya, West Nile Virus na Rift Valley Fever.***

**Ndugu Wananchi**

Katika kuongeza wigo wa utambuzi wa chanzo cha ugonjwa huu, uchunguzi katika Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali umefanyika ili kubaini uwezekano wa kuwa na sumu au kemikali zinazoathiri Afya ya Binadamu. Majibu kutoka maabara hii yameonesha kuwa, hakuna sumu au kemikali yoyote yenye uwezekano wa kuathiri afya ya binadamu.

**Ndugu Wananchi**

Nachukua fursa hii kuwataarifu kuwa, kwa sasa upimaji wa sampuli za wagonjwa kutoka maabara zetu umethibitisha mlipuko huu kuwa wa ugonjwa wa **Leptospirosis, Field Fever (na kwa lugha ya Kiswahili inajulikana kama**

**Homa ya Mgunda)**. Leptospirosis ni miongoni mwa magonjwa yanayoambukizwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu na unasababishwa na Bakteria aina ya *Leptospira interrogans*. Ugonjwa huu umekuwepo katika maeneo ya kitropiki ambayo ni yenye hali ya joto katika mabara ya Amerika ya Kaskazini, Amerika ya Kusini, Afrika, Asia na Australia. Wanyama aina za panya, kindi, mbweha, kulungu, swala, na wanyamapori wengine wameripotiwa kupata maambukizi ya vimelea hivi na kuwa chanzo cha maambukizi kwa binadamu. Kwa Tanzania, ugonjwa huu si mpya, na ulishawahi kutokea mwaka 2014 katika Halmashauri ya Buhigwe mkoani Kigoma.

**Ndugu wananchi**

Ugonjwa wa Leptospirosis huambukizwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu kupitia uchafuzi wa mazingira ikiwemo vyanzo vya maji kutoka katika mkojo wa wanyama wenye maambukizi. Maambukizi ya ugonjwa huu kwenda kwa binadamu hupitia njia zifuatazo;

i. Kugusa mkojo (au maji maji mengine ya mwili) kutoka kwa wanyama wenye maambukizi.
ii. Kugusa maji, udongo, au chakula kilichochafuliwa na mkojo wa wanyama wenye maambukizi.
iii. Kunywa maji yaliyochafuliwa na vimelea vya bakteria wa ugonjwa huu

Aidha, bakteria wanaweza pia kuingia mwilini kupitia ngozi au utando wa *mucous* (macho, pua au mdomo) na kupitia ngozi yenye mikwaruzo. Maambukizi ya ugonjwa huu kutoka kwa binadamu mmoja kwenda kwa mwingine hutokea kwa nadra.

**Ndugu Wananchi**

Mgonjwa aliyeambukizwa vimelea vya ugonjwa huu huanza kuonesha dalili katika kipindi cha kati ya siku tano (5) hadi 14 na wakati mwingine dalili huweza kutokea kati ya siku mbili (2) hadi 30. Dalili za ugonjwa huu zinajumuisha homa,

kuumwa kichwa, maumivu ya misuli, uchovu wa mwili, mwili kuwa na rangi ya manjano, macho kuvilia damu, kutoka damu puani pamoja na kukohoa damu.

**Ndugu Wananchi,**

Serikali kupitia Wizara ya Afya na wadau wengine imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kama ifuatavyo:

i. Kutafuta watu wengine wenye dalili ili kuwapatia huduma
ii. Kutoa huduma kwa wagonjwa pindi wanapojitokeza
iii. Kuwezesha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vifaa vya kujikinga na maambukizi
iv. Kutekeleza dhana ya Afya Moja (One Health Concept) kwa kuwashirikisha wataalam wa Mifugo, Wanyama pori, Kilimo na Mazingira katika kudhibiti ugonjwa huu
v. Kutoa mwongozo wa kitaalam wa jinsi ya kubaini wagonjwa zaidi na kuwahudumia
vi. Kutoa elimu kwa jamii ili kujikinga dhidi ya ugonjwa huu

**Ndugu Wananchi,**

Kwa bahati nzuri ugonjwa huu unaweza kuzuilika na unatibika. Wizara inatoa wito kwa watu wote kuzingatia yafuatayo:

i. Kuchukua hatua zote stahiki za kujikinga na ugonjwa huu ikiwemo kuepuka kugusa maji au vitu vilivyochafuliwa na mkojo wa wanyama na kunywa maji safi na salama ambayo yamechemshwa au kutibiwa

ii. Wagonjwa wenye dalili za homa, kuvuja damu, kichwa kuuma na mwili kuchoka kwenda kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ili wapate matibabu sahihi

iii. Kutoa taarifa za wagonjwa wanaoonesha dalili zilizotajwa hapo juu endapo watabainika kuwepo ndani ya jamii

Kabla ya kuhitimisha nipende kutoa pongezi kwa Wataalam wetu wa Afya ngazi ya Halmashauri ya Ruangwa na Mkoa wa Lindi kwa kushirikiana na viongozi wao, jinsi walivyoweza kubaini kwa haraka tishio hili na kutoa taarifa mapema. Hii inaonesha jinsi eneo la Ufuatiliaji wa Magonjwa (Disease Surveillance) lilivyoimarishwa, endeleeni na utaratibu huo na hii iwe kwa nchi nzima. Aidha, nawapongeza wataalam wote kutoka taasisi mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa walioshiriki katika ufuatiliaji wa ugonjwa huu.

**Hitimisho**

**Ndugu wananchi**

Wizara inaendelea kuchukua hatua za kukabiliana na ugonjwa huu na kuendelea kutoa taarifa kwa umma kuhusu mwenendo wa ugonjwa huu. Hivyo Serikali inawaasa Wananchi kutokuwa na hofu kwani ugonjwa huu unaendelea kudhibitiwa.

**Imetolewa na;**

**Ummy A. Mwalimu (Mb)**

**WAZIRI WA AFYA**